

## TAARIFA NA HUDUMA ZA MAELEKEZO KUHUSU ENEO

Taarifa za makaribisho zinazotoa maelezo kuhusu huduma na vistawishi katika eneo lako na maelezo kuhusu utamaduni. Vipindi vya kutoa maelekezo ili kuwasaidia wahamiaji kuelewa jamii, sheria na desturi za eneo lao.

## USAIDIZI WA LUGHA

Mafunzo au nyenzo za lugha za kuwasaidia wahamiaji kuboresha ujuzi wao wa Kiingereza. Huduma za tafsiri kwa hati na mawasiliano muhimu.

## USAIDIZI WA KISHERIA

Ushauri na usaidizi wa kisheria kuhusiana na masuala ya uhamiaji. Maelezo kuhusu haki na majukumu. Shirika la Family Promise Marekani kwa sasa limo katika mchakato wa kuomba litambumbuliwe na kuidhinishwa na Idara ya Haki kutoa uwakilishi wa kisheria katika kesi za uhamiaji.

## MAKAZI YA DHARURA NA MAHITAJI YA MSINGI

Usaidizi wa mahitaji ya msingi - makazi ya dharura, chakula, mavazi, bidhaa za matumizi, fanicha, usaidizi wa kodi ya nyumba, usaidizi wa gharama za huduma za umma na mahitaji mengine ili kuleta au kudumisha uthabiti.

## USAIDIZI WA AJIRA

Usaidizi wa kutafuta kazi, warsha za mafunzo ya kuandika wasifu kazi na matayarisho ya mahojiano ya kazi. Taarifa kuhusu maonyesho ya kazi na nafasi za ajira katika eneo lako.

## USAIDIZI WA MAKAZI

Maelekezo ya jinsi ya kupata makazi nafuu. Usaidizi wa kifedha unapopatikana. Maelezo kuhusu haki na majukumu ya wapangaji.

## MAELEZO YA HUDUMA ZA AFYA

Maelekezo kuhusu jinsi ya kupata huduma za afya. Maelezo kuhusu chaguo za bima ya afya na huduma nafuu au zisizolipishwa.

## NYENZO ZA ELIMU

Maelezo kuhusu shule, vyuo na mipango ya elimu kwa watu wazima katika eneo lako. Usaidizi kuhusiana na utaratibu wa kujiandikisha.

## MIPANGO YA UTAMADUNI NA JAMII

Hafla na mipango inayosherehekea tamaduni tofauti tofauti. Juhudi za ujumuishaji katika jamii, kama vile mipango ya kubadilishana maarifa ya tamaduni.

## HUDUMA ZA JAMII

Ufikiaji wa huduma za usaidizi wa jamii, ikiwa ni pamoja na ushauri na nyenzo za afya ya akili. Maelezo kuhusu jamii na vikundi vya kijamii katika eneo lako.

## USAIDIZI WAKATI WA MAJERAHA

Mipango maalum na usaidizi kwa wanawake na watoto wahamiaji ambao wameathirika na ulanguzi, wamedhulumiwa au kujeruhiwa.

## NAFASI ZA KUFHAMIANA

Mikutano au matukio ya kuwasaidia wahamiaji kufahamiana wenyewe na jamii katika eneo lao. Mipango ya ushauri inayounganisha wageni na wakaazi wa muda mrefu.

## USAIDIZI KUHUSIANA NA SERIKALI NA UTAWALA

Usaidizi wa jinsi ya kupata huduma na hati za serikali. Maelezo kuhusu nyenzo za jamii na za serikali katika eneo lako.

## TAARIFA KUHUSU USAFIRI

Maelezo kuhusu jinsi ya kupata leseni za udereva na usajili wa magari. Usaidizi wa usafiri (gari la FP au Uber) kwa muda mfupi.

## MIPANGO YA MAFUNZO YA KIFEDHA

Warsha kuhusu kufanya bajeti, masuala ya benki na upangaji wa fedha. Taarifa kuhusu mipango inayopatikana ya usaidizi wa kifedha.

## MAWASILIANO NA UTETEZI WA JAMII

Utetezi wa haki na uwakilishi wa wahamiaji. Miradi ya kuifikia jamii ili kukuza uelewa na ujumuishaji.

## HUDUMA ZA UTUNZAJI WA WATOTO

Maelezo kuhusu chaguo za utunzaji wa watoto katika eneo lako. Kuwekwa katika mpango wa Family Promise wa utunzaji wa watoto unapopatikana. Usaidizi wa kuwaandikisha watoto shuleni.

## MAWASILIANO

★ **MAHALI TULIPO:** 201 W. Main Street, Level 3, Plainfield, IN 46168

★ **SIMU:** 317-296-3742

★ **BARUA PEPE:** INFO@FamilyPromiseHendricksCounty.org

★ **WAFANYAKAZI:** Mariela Lozano: Mkurugenzi wa Uhamiaji - Mariela@FamilyPromiseHendricksCounty.org  
Carlos Murillo: Wakili wa Uhamiaji - Carlos@FamilyPromiseHendricksCounty.org  
Jorge Portillo: Wakili - JorgeP@FamilyPromiseHendricksCounty.org  
Katy Beringer: Mratibu wa Elimu - Katy @FamilyPromiseHendricksCounty.org

★ **MIADI:** Tafadhali piga simu au tuma barua pepe kuweka miadi ya kupata usaidizi. Asante!

